BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA 0FISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia uhai na afya njema, tukaweza kukutana tena katika Baraza hili Tukufu kwa lengo la kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali kwa niaba yao ambapo leo tupo hapa kuijadili Bajeti ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kutujaalia nguvu na imani tuweze kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa hekima na uadilifu mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Natoa shukuran zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipa fursa hii kusimama mbele ya Baraza lako kwa niaba ya Kamati ya Bajeti kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati yangu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Pongezi za kipekee ziende kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni sikivu, chini ya uongozi imara wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza La Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, kwa namna anavyozitekeleza vyema ahadi zake alizozitoa katika uongozi wake kwa kutuletea maendeleo pamoja na kuimarisha uchumi wa Zanzibar akiwa na mashirikiano makubwa na wasaidizi wake Makamo wa Kwanza, Mhe. Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili, Mhe. Hemed Suleiman Abdullah.

**Mheshimiwa Spika**,

Kamati inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango kwa uongozi wao madhubuti ambao umewafanya Watendaji wote wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuwa na mashirikiano mazuri yaliyoiwezesha Kamati ya Bajeti kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Ni imani yetu kuwa, mashirikiano haya yatazidi kuimarika siku hadi siku na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Bajeti imefanya kazi ya kuchambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 kupitia mafungu yake yote, kuanzia Fungu F01 hadi F07. Msingi wa Hotuba huu ni matakwa ya fasili ya 97(1) ya kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020).

**Mheshimiwa Spika,**

Kukamilika kwa Hotuba hii kwa kiasi kikubwa kumetokana na michango ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti. Hivyo, napenda kuwapongeza kwa dhati kwa mashirikiano yao yaliyopelekea kutekeleza majukumu yetu kwa umahiri wa hali ya juu kwa kushirikiana na makatibu wetu. Kwa ruhusa yako naomba sasa niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan | Makamo Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Asha Abdalla Mussa | Mjumbe |
| 4. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 5. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |
| 6. Mhe. Rukia Omar Ramadhan | Mjumbe |
| 7. Mhe Suleiman Masoud Makame | Mjumbe |
| 8. Mhe. Yussuf Hassan Iddi | Mjumbe |
| 9. Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 10. Ndg. Abass Vuai Mohammed | Katibu |
| 11. Ndg. Husna Rajab Othman | Katibu |
| 12. Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango imejumuisha mafungu makuu saba (7) ambayo ni Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango F01, Mfuko Mkuu wa Serikali

F02, Tume ya Mipango F03, Ofisiya Mtakwimu Mkuu wa Serikali F04, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali F05, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani F06 na Ofisi ya Msajili wa Hazina F07.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango imekadiriwa kukusanya TZS 4.901 trilioni sawa na ongezeko la asilimia 77 ya makadirio ya kukusanya TZS 2.767 trilioni kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**,

Mapato ya Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango yamejumuisha mapato ambayo yanakusanywa na Taasisi zake kuu za ukusanyaji wa mapato nchini ambazo ni Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Kamati ilipokea taarifa ya kupanda kwa makusanyo hayo katika kipindi cha miezi tisa Julai – Machi, 2024 ambapo ZRA ilikusanya TZS 559.484 bilioni sawa na asilimia 117 ya makadirio ya kukusanya TZS 479.178 bilioni. Mapato hayo yameongezeka kwa asilimia 25 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya kodi ya miezi tisa ya mwaka 2022/2023 ambayo yalikuwa TZS 449.283 bilioni. Aidha, kwa kipindi hicho cha tathmini, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa upande wa Zanzibar imekusanya jumla ya TZS 384.366 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kukusanya TZS 383.978 bilioni ikiwa ni ongezeko la asilimia 18 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya kodi ya miezi tisa ya mwaka 2022/2023 ambayo yaliyokuwa TZS 325.611 bilioni. Kamati ya Bajeti inazipongeza Taasisi hizi kwa hatua hii iliyofikia ambayo inatokana na juhudi za watendaji pamoja na uimarishaji wa mifumo ya ukusanyaji wa

mapato.

**Mheshimwa Spika,**

Licha ya ongezeko hilo la ukusanyaji wa mapato kwa mwaka 2023/2024, bado kulikuwa na uchache wa upatikanaji wa fedha za uwendeshaji katika baadhi ya Wizara na Taasisi ambazo kamati ilipata bahati ya kuzipitia wakati wa mizunguko yake ya kiutendaji zikiwemo zile zilizo chini ya Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango. Hivyo, ni matumaini ya Kamati kuwa bajeti ambayo itakwenda kuidhinishwa ya mwaka wa fedha 2024/2025 itaweza kutatua changamoto hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilipokutana na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ilipitia mafungu yote saba ya Ofisi hii ambapo kupitia mafungu hayo majukumu ya kila siku ya Ofisi hii yatatekelezwa. Kamati ilipata fursa ya kuyapitia kwa kina mafungu yote kwa upande wa mapato, matumizi pamoja na Miradi na Programu zake. Kwa muktadha huo naomba sasa nitoe maoni ya Kamati ya Bajeti kama ifuatavyo:

## FUNGU F01 - (OR-FEDHA NA MIPANGO)

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati wakati wa kuyapitia mafungu, iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu **F01** linakadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 2.981 trilioni**. Aidha, kwa kuwa makusanyo yaliyopangwa katika fungu hili yameongezeka kutoka **TZS 1.945 trilioni** za mwaka 2023/2024, Kamati inaipongeza Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa makadirio haya kwani fedha hizi zitakapokusanywa kwa kiwango kilichopangwa zitasaidia kuongeza

mapato yetu.

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa upande wa matumizi, Fungu **FO1** limekadiriwa kutumia jumla ya **TZS 665.392 bilioni** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake za msingi. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kukusanya na kutumia fedha hizo kwa mujibu wa Programu zilizopangwa na kama inavyoelekeza kwenye Sheria Na. 11 ya ununuzi na Sheria Na. 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika,**

Mapato ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi yaliyo chini ya kifungu **F0106** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yamepangiwa jumla ya **TZS 25.0 bilioni** ikiwa ni kwa ajili ya ununuzi wa gari ambapo Taasisi zote zinazojitegemea zinatakiwa kuleta maombi ya ununuzi wa gari katika Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango. Kamati inaipongeza Ofisi kwa hatua hii ambayo itakwenda kuleta suluhisho la uchache wa vyombo vya usafiri ikiwemo gari katika baadhi ya Taasisi.

**Mheshimiwa Spika**,

Mapato ya Idara ya Uhamiaji yaliyopo chini ya Kifungu **F0126** yanakadiriwa kuongezeka kutoka **TZS 75.0 bilioni** hadi kufikia jumla ya **TZS 92.5 bilioni** kwa mwaka 2024/2025. Kamati iliarifiwa kuwa mapato hayo yametokana na ongezeko la makusanyo ya shughuli za uhamiaji yakiwemo Ada ya hati ya kusafiria ya kawaida, Ada ya hati ya kusafiria ya Kidiplomasia pamoja na kuongezeka kwa ruhusa ya ukaazi kwa wanafunzi. Kamati inaendelea kuipongeza Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kupitia Idara ya Uhamiaji kwa

kuendelea kusimamia vyema ukusanyaji wa mapato kwa maeneo waliyopangiwa na ambayo yana mchango mkubwa kwenye Mfuko Mkuu.

## PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA BAJETI NA FEDHA ZA UMMA

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali iliyo chini ya kifungu **SF010102** inakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 134.047 bilioni** ikilinganishwa na fedha zilizotengwa kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2023/2024 ambazo zilikuwa jumla ya **TZS 87.177 bilioni**. Kamati inaipongeza Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kuongeza fedha katika Programu hii ambayo itakwenda kuleta ufanisi wa kusimamia utayarishaji wa Bajeti ya Serikali, Utayarishaji wa mabadiliko ya miongozo na sera za bajeti pamoja na ufuatiliaji wa bajeti katika Taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ndogo ya **SF010401** ya Uendeshaji na Utumishi inakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 33.016 bilioni** ukilinganisha na fedha zilizotengwa kwa mwaka 2023/2024 ambazo ni **TZS 5.714 bilioni**. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha katika fungu hili ili kutatua changamoto ya ukosefu wa vifaa vya kutendea kazi, kuendelea na shughuli ya usimamizi wa rasilimali watu ili kuleta ufanisi katika kazi.

## FUNGU F02 - MFUKO MKUU WA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, kifungu cha **PF0201** cha Program Kuu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali, fedha zilizotengwa zimeongezeka kutoka **TZS 258.449 bilioni** na kufikia **TZS 416.897 bilioni**. Kamati inaunga mkono ongezeko hili pamoja na kuishauri Serikali kupitia Program hii kuhakikisha kuzidisha nidhamu katika matumizi ya fedha za umma. Aidha, Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa matumizi yake yote yanayofanywa, hasa yale yanayohusiana na ulipaji wa madeni, hayaainishwi na kuhesabiwa katika fungu jengine lolote ili kufanya matumizi mazuri ya fedha.

## FUNGU F03 TUME YA MIPANGO

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 makadirio yaliyopangwa katika fungu la Tume ya Mipango ni **TZS 11.766 bilioni**. Kamati inakubaliana na makadirio hayo pamoja na kuishauri na kuitaka Serikali kuipatia Tume fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kama ilivyojipangia. Kwa kuwa upatikanaji wa fedha katika Tume hii kutapelekea utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi ikiwemo kuandaa mipango ya Maendeleo pamoja na kuratibu utekelezaji na ufuatialiaji wa mipango hiyo kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**,

Jukumu jengine la Tume ya Mipango ni kufanya tafiti katika masuala yenye maslahi ya Taifa na Sera za Kijamii. Kwa vile tafiti ni suala muhimu katika maendeleo ya nchi, ni matarajio ya Kamati ya Bajeti kuwa Tume itaendelea kuwezeshwa vyema kifedha na kitaalamu katika kufanikisha majukumu yake ikiwemo ufanyaji wa tafiti hizo.

## PROGRAMU YA KURATIBU MIPANGO YA KITAIFA NA MAENDELEO YA WATENDA KAZI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini **(SF030101**) inakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 3.473 bilioni** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025. Kiasi hichi ni kidogo ukilinganisha na fedha zilizoizidhinishwa mwaka 2023/2024 ambazo ni jumla ya **TZS 4.419 bilioni.** Kamati inapata wasi wasi juu ya upungufu wa fedha katika Programu hii hasa ukizingatia kuwa fedha zinahitajika katika kuimarisha uratibu wa mipango ya maendeleo ya Kitaifa, kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mipango hiyo pamoja na kuratibu masuala ya hali ya umasikini Zanzibar. Hata hivyo, kwa kuwa utafiti wa kitaifa kuhusiana na mahitaji na uwezo wa watendakazi ulifanyika mwaka 2023/2024, Kamati imekubaliana na upungufu huo wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa shughuli zinazotekeelzwa katika programu hii ni kujenga uelewa wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 kwa makundi na Taasisi mbali mbali Unguja na Pemba pamoja na kufanya vipindi vya Redio na Televisheni ili kujenga uelewa wa Dira hiyo kwa wananchi. Kwa mantiki hiyo, ni busara fedha zake kupatikana kikamilifu na kwa wakati ili kuweza kufikia malengo ya Programu hii.

## FUNGU F04 – OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,**

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ni taasisi inayojitegemea ambayo imeanzishwa kwa Sheria ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Nam. 9 ya 2007 ikiwa na dhamana ya kuendeleza, kuratibu na kutunza takwimu rasmi Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, Fungu **F04** linalosimamiwa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali linakadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 0.134 bilioni** na kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, fungu hilo linakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 13.113 bilioni** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake.

**Mheshimiwa Spika,**

Ofisi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake, Kamati inashauri Serikali kuipatia fedha kwa mujibu wa zilivyoidhinishwa na Baraza. Aidha, suala la kupatiwa wataalamu na kuendeleza wafanyakazi waliopo katika uandaaji wa nyenzo za kufanyia utafiti kwa mujibu wa mahitaji yao kutasaidia sana kuimarisha utendaji wao wa kazi. Vile vile, upatikanaji wa vitendea kazi za kitakwimu ikiwemo gari kwa ajili ya kufanya kazi za nje (field) kutapelekea ofisi hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

## FUNGU F05 - OFISI YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025, fungu **F05** linalosimamiwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali linakadiriwa kukusanya jumla **TZS 1.884 trilioni** na kuchangia kwenye mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, fungu hilo linakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 14.754 bilioni** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake za msingi.. Hivyo, Kamati inatoa pongezi kwa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa kulipangia fungu hili nyongeza ya fedha

ambazo zitasaidia katika utekelezaji bora wa majukumu yake, yakiwemo yale ya usimamizi wa hazina ambayo ni chachu ya maendeleo ya Taifa letu.

## FUNGU F06 - OFISI YA MKAGUZI MKUU WA NDANI WA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,** Ieleweke kuwa Ukaguzi wa ndani wa hesabu ni suala la msingi sana katika utekelezaji wa dhana nzima ya utawala bora. Jukumu hilo kwa hapa Zanzibar linasimamiwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa ndani wa Serikali. Kwa mwaka wa fedha **2024/2025**, fungu **F06** linalosimamiwa na Mkaguzi Mkuu wa ndani wa Serikali linakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 6.069 bilioni** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake. Kamati inashauri Ofisi kuingiziwa fedha kwa ukamilifu na kwa wakati ili kuongeza ufanisi na ubora wa kazi zake.

## FUNGU F07 OFISI YA MSAJILI WA HAZINA

**Mheshimiwa Spika,**

Ofisi ya Msajili wa Hazina ni fungu jipya katika Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 fedha zilizokadiriwa katika fungu hili ni **TZS 5.219 bilioni** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Kwa kuzingatia upya wa fungu hili, Kamati inaishauri Ofisi ya Msajili wa Hazina kuhakikisha fedha walizotengewa wanazitumia vyema katika kutekeleza programu zao ikiwemo kufanya usimamizi mzuri wa mali za umma na uwekezaji wa Mashirika ya Umma ili hatimae malengo ya kuanzishwa kwa fungu hili yaweze kufikiwa kwa ufanisi.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati hii ina imani kubwa na Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango na inatarajia kuimarika kwa upatikanaji wa fedha za kutosha za matumizi ya kawaida ili kuimarisha utekelezaji wa Bajeti Kuu ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kuwa Kamati yangu imejadili kwa kina na kuyakubali makadairio ya mapato na matumizi kwa mafungu makuu saba ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2024/2025 sambamba na shabaha zake, naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waipitishe Bajeti hii ili shughuli zilizopangwa kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 ziweze kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati ya Bajeti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

.............................................

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**